**Waziri wa zamani ahukumiwa kifungo kwa Makosa ya Rushwa**

***Na Mussa Misalaba, kwa msaada wa mashirika ya habari ya kimataifa***

Watu 22, akiwemo mwenyekiti wa zamani wa bodi ya wakurugenzi wa kampuni kubwa ya mafuta na gesi vietinam - PVN, Dinh La Thang, wamehukumiwa na mahakama ya Hanoi , kwenda jela kutokana na kupatikana na hatia ya makosa ya matumizi mabaya ya madaraka , ubadhirifu na kuisababishia hasara serikali , vyombo vya habari vya kimataifa vimeripoti.

Thang na wenzake 21 walihukumiwa jumatatu Januari 22, 2018 asubuhi kutumikia vifungo virefu jela kufuatia kesi iliyofunguliwa na serikali ya Vietnam Januari 8 mwaka huu kuhusiana na matumizi mabaya ya madaraka , ubadhirifu na kuisababishia hasara kubwa serikali kwenye kampuni ya PVC iliyokuwa inasimamia na kutekeleza mradi wa umeme wa Thai Binh 2.

Mahakama ya Hanoi, mji mkuu wa Vietnam, ilimhukumu Thang kifungo cha miaka 13 jela huku Mkurugenzi Mkuu na Mwenyekiti wa zamani wa Bodi ya Wakurugenzi wa PVC ,Trinh Xuan Thanh, akihukumiwa kifungo cha maisha jela. Washtakiwa wengine 20 walihukumiwa vifungo vya hadi miaka 22 jela.



*Trinh Xuan Thanh***,** Mkurugenzi Mkuu na Mwenyekiti wa zamani wa Bodi ya Wakurugenzi wa PVC *akisindikizwa na polisi kuelekea kwenye gerezani kutumikia kifungo chake cha maisha*

Mshtakiwa mwingine wa ngazi za juu kwenye kampuni ya PVCaliyetiwa hatiani na kuhukumiwa kwenda jela ni aliyekuwa mkurugenzi mkuu wa kampuni ya PVC ambayo ni kampuni tanzu ya PVN, ni Vu Duc Thuan. Alihukumiwa kutumikia jela miaka 9.

Thang mwenye umri wa miaka 57 alitenda makosa haya kati ya mwaka 2006 na 2011 alipokuwa Katibu wa kamati kuu ya chama tawala na Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi wa kampuni kubwa ya mafuta na gesi ya Vietanam ( Petro Vietnam, PVN kwa kifupi).



**Dinh La Thang, Mwenyekiti wa zamani wa PVN aliyefungwa jela miaka 13**

Oktoba 2007, wizara ya Viwanda na Biashara iliipa kazi PVN kuendeleza ujenzi wa mradi wa umeme wa Thai Binh 2 . Juni 18,2010 bila kufuata taratibu za zabuni Thang alisaini maazimio ya PVN kwamba PVC, ambayo ni kampuni tanzu ya ujenzi ya PVN, itekeleze kazi ya uhandisi, manunuzi na ujenzi (EPC) wa mradi wa umeme wa Thai Binh 2 kwa mtaji wa VND 31.5 trioni ($1.7 bilioni) bila kuzingatia uwezo na uzoefu wa kampuni hii.

Katika hatua nyingine , Thang aliiagiza PVN kuilipa PVC malipo ya awali zaidi ya $6.6 milioni na VDN 1.3 trilioni ($ 59 milioni) katika utekelezaji wa mkataba huu kinyume na kanuni za serikali za usimamizi wa uchumi.

Trinh Xuan Thanh na Vu Duc Thuan, mkurugenzi mkuu wa zamani wa PVC, walisaini mkataba wa EPC mbali ya kupokea malipo ya awali katika utekelezaji wa mkataba huu, zaidi ya $6.6 milioni na VDN 1.1 trilioni ($48.4 milioni). Thanh alitumia vibaya sehemu ya malipo ya awali, VDN 1.1 trilioni ($48.4 milioni), kwa matumizi mengine yasiyokusudiwa hivyo kuisababishia hasara kubwa serikali.

Upande wa mashtaka ulieleza mahakama kuwa karibu fedha zote zilizotolewa kama malipo ya awali katika utekelezaji wa mradi wa umeme wa Thai Binh 2 zilitumika kulipia madeni ya PVC kwenye mabenki na zingine ziliwekezwa kwenye makampuni tanzu na miradi mingine.

Mahakama ya Hanoi ilimtia hatiani Thang baada ya kuridhika kuwa anahusika na makosa yaliyotendwa na Thanh yaliyosababisha upotevu wa zaidi ya VND119bilioni($5.24 milioni katika mradi wa umeme wa Thai Binh 2 na ubadhirifu wa VND 4 billion ($176,000) za mradi mwingine wa umeme unaomilikiwa na kuendeshwa na PVN, Vung Ang – Quang Trach.

Thang alikuwa akiwaagiza watumishi waliokuwa chini yake kusaini mikataba kinyume na kanuni na hivyo kumwezesha Trinh Xuan Thanh kujichotea fedha hizo kwa matumizi yake mabaya yasiyokusudiwa.

Thanh na Thuan, waliteuliwa na Thang, wakati akiwa mwenyekiti wa PVN, kwa misingi ya urafiki toka ngazi za chini kabisa bila kuwa na uzoefu wa nafasi walizoteuliwa.

Thanh aliweza kujichotea VDN 4 bilioni (176,000) kwenye mradi wa umeme wa Vung Ang – Quang baada ya kutengeneza nyaraka za uwongo kwa kushirikiana na wafanyanyakazi wengine waliokuwa chini yake kuongeza gharama za ujenzi kwa kiasi cha VND 13 bilioni ($572,456 ) ambazo aligawana na maswahiba wake. Vu Duc Thuan, mkurugenzi mkuu wa zamani wa PVC, ambaye alijipatia VND 800 MILIONI ($ 35,228).

Mbali na kesi ya sakata la PVN, Thang anakabiliwa na kesi nyingine inayohusiana na matumizi mabaya ya madaraka , na kuisababishia hasara kubwa serikali kutokana na uwekezaji wa ovyo alioufanya kwenye benki ya Ocean iliyokuwa na hali mbaya kifedha na kiuendeshaji na anaweza kuhukumiwa kifungo cha hadi miaka 20 jela.

Mwaka 2008 Thang akiwa mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa PVN alisaini mkataba ambao uliiwezesha PVN kuwa mbia na mwekezaji wa kimkakati kwenye

Ocean Bank kwa kuwekeza kwa hasara VND 800 bilioni (US $35.24 milioni), sawa na 20% ya hisa zote kinyume na kanuni za nchi katika udhibiti wa uchumi.

Licha ya kwamba mwaka 2008 benki ya Ocean ilikuwa na utendaji mdogo na mbovu Thang hakujali na aliendelea na mipango yake ya uwekezaji kwa kununua 20% ya hisa zote na bila kuifanyia tathmin na bila kutoa taarifa kwa waziri mkuu.PVN ilipoteza fedha zote ilizowekeza kwenye benki ya Ocean baada ya benki kuu ya Vietnam kuamua kuinunua bila malipo mwaka 2015.

Pamoja na kumalizika kwa kesi hii, Thanh anakabiliwa na kesi nyingine kubwa ya ubadhirifu wa $622,000 za mradi mwingine wa ujenzi kwenye kampuni ya PVPL,kampuni tanzu ya PVN na anaweza kuhukumiwa adhabu ya kifo kwa mujibu wa sheria za Vietnam. Kesi ilifunguliwa Januari 24, mwaka huu kwenye mahakama kuu ya Hanoi.

Thang alikuwa nyota inayochomoza kwa kasi kwenye ulingo wa siasa za Vietnam na alikuwa maarufu sana. Kati ya mwaka 2006 na 2011 Thang alikuwa mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi wa PVN kabla ya kuwa waziri wa usafirishaji katika baraza la mawaziri la waziri mkuu Nguyen Tan Dung na baadaye kiongozi wa chama tawala jiji la Ho Chi Minh.

Kufuatia tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka Thang alianza kuonja joto la jiwe Mwezi Mei 7, 2017 alipoondolewa kwa kura kwenye nafasi yake ya ujumbe wa kamati kuu ya chama yenye wajumbe 19 yenye jukumu la kufanya maamuzi. Baadaye alikuja kuondolewa kwenye nafasi yake ya uongozi wa jiji la Ho Chi Minh kabla ya kuvuliwa uanachama Desemba 8,mwaka jana baada ya kukamatwa na polisi.

Kwa hivi sasa Vietnam inaendelea na usafishaji wa vitendo vya rushwa kote nchini kwa kuanzia na sekta za nishati na benki na watu wengi wameshakamatwa na kufikishwa mahakamani kwa kutumia sheria yake ya jinai iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2015 na kuanza kutumika January 1, 2018.